TARGETER WINGS
JUNIOR SCHOOL ASSESSMENT
GREDI YA NANE - 2024
KISWAHILI

Wings 006

Muda: Saa 1 dakika 20

Jina	
Shule	
Nambari ya Usajili:	**Tarehe**

Maagizo

(a) Andika jina lako, la shule, nambari ya usajili na tarehe kwenye vihasho uliopewa.

(b) Jibu maswali yote kwenye karatasi hili.

MTAHINI PEKEE			
Swali	**Upeo wa alama**	**Alama ya mwanafunzi**	**Kiwango cha utendaji**
1-29	Alama 50		
Jumla	**50**		

I. UFAHAMU WA KUSOMA

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la 1 hadi 4:

Hapo zamani, Sungura na Fisi walikuwa marafiki wa chanda na pete. Walizama na kuibuka pamoja katika shughuli mbalimbali za maisha. Marafiki hawa walilea familia zao pamoja. Walifanya kazi kwa ushirikiano shambani. Mvua nayo ilinyesha msimu baada ya mwingine. Mashamba yao yalinawiri na maghala yao yakaanza kulalamikia shibe. Pia walichunga mifugo wao pamoja.

Watoto wa sungura na Fisi walicheza pamoja bila kujali tofauti zao za kimaumbile. Kila siku, waliamka alfajiri kwenda kuchunga mifugo ya wazazi wao. Kadri siku zilivyosonga, ndivyo urafiki wao ulivyozidi kuwa imara. Udugu kati ya familia hizi mbili uliimarika zaidi.

Hata hivyo, siku za mazuri zilianza kubishwa na maovu. Mvua ilikataa katakata kukitembelea kijiji chao. Akiba ya chakula kilichokuwa ghalani kikaanza kupungua na hatimaye kikaisha kabisa.

Fisi alilala kitandani akiwa mwenye mawazo tele. Hali ya baadaye ya familia hizi mbili ilianza kuwa mbaya. Aliogopa kuwa wanao wangegeuka magofu. ***Asubuhi moja baada ya familia yake kula mate usiku uliotangulia***, alimwendea sungura kwa ushauri wa namna ya kukabiliana na hali mbaya iliyowapata.

Baada ya kuwaza na kuwazua, wazo zuri lilimjia sungura "kaka yangu, janga hili la njaa ni tokeo la hasira za mizimu. Mababu zetu walikosa nasi hatuna budi kuangukiwa na laana za mizimu. Juzi usiku, mizimu ilinijia ndotoni. Iliniambia kwamba njia ya pekee ya kujiopoa na familia zetu ni kwa kuituliza kwa kuitolea kafara. Tukifanya hivyo, mvua itanyesha na tutaweza kuyanusuru maisha ya familia zetu."

1. Kwa nini Fisi na Sungura walivuna mazao mengi?

_____

2. Ni jambo gani lililosababisha upungufu wa chakula ghalani?

_____

3. Andika maana ya kauli: "asubuhi moja baada ya familia yake kula mate usiku uliotangulia"

_____

4. Njia ya pekee ya kunusuru familia za Fisi na Sungura ilikuwa ni kuitolea mizimu kafara kwa mujibu wa Sungura. Andika kauli kuthibitisha kuwa kauli hii si ya kweli.

_____